



## BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

### ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

#### BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

#### MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 31 Mei, 2022**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua zitasomwa.

#### I. MASWALI:

##### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

134. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)  
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala  
za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ni jambo la kupon gezwa kwamba, hivi karibuni Serikali imeasisi  
au/na kurekebisha baadhi ya posho kwa ajili ya watumishi wa  
Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU). Hata hivyo, kumekuwa na  
malalamiko makubwa kutoka kwa baadhi ya watumishi wa JKU  
kwamba posho hizo zimewazingatia watumishi wa ngazi za juu  
tu na kuwaacha wengine bila kufikiriwa maslahi hayo mapya.

- (a) Je, ni posho gani zilizoasisiwa au/na kurekebishwa ndani  
ya mwaka huu wa fedha wa 2021/2022 katika Jeshi la  
Kujenga Uchumi (JKU) na kwa watumishi wa ngazi zipi.
- (b) Je, ni kwa nini watumishi wa ngazi za chini wameachwa  
katika marekebiso hayo.
- (c) Je, ni lini posho mpya zitaasisiwa na za zamani  
kurekebishwa kwa watumishi wa ngazi za chini wa Jeshi  
la Kujenga Uchumi (JKU).

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

81. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Serikali nyingi duniani huweka hisa zake katika Kampuni mbali mbali ndani na nje ya nchi kwa dhamira ya kukuza mapato yake.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewekeza katika Kampuni ngapi ndani na nje ya Zanzibar.

**Wizara ya Afya:**

111. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la waganga wa kienyeji pamoja na watu wanaojishughulisha na tiba mbadala, na kwa kuwa wananchi wengi wamevutika na matumizi ya dawa hizo ambazo nyingi zimekosa viwango pamoja na vipimo katika mafunzo yake, jambo ambalo linaweza kusababisha madhara makubwa kwa afya ya binadamu.

Je, Serikali inachukuwa hatua gani kudhibiti matumizi ya dawa za asili zisizokuwa na vipimo wala viwango.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

94. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Asilimia kubwa ya nchi nyingi duniani hujengwa kumbi maalum kwa ajili ya mikutano ya Kimataifa. Pamoja na mambo mengine uwepo wa kumbi hizo kunachochea pia Serikali kupata mapato kupitia wageni mbali mbali watakaoshiriki mikutano ya Kimataifa kwa kutembelea maeneo tofauti ya kitalii.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango gani wa kujenga kumbi za Kimataifa hapa Zanzibar.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

140. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)  
 - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika kuboresha huduma za maji, Serikali hutoza kiwango cha fedha kulingana na matumizi yatakayosomwa na mita au kwa bei ya shilingi 4,000/= kwa mwezi kwa watumiaji wasio na mita. Hata hivyo, kwa wananchi na wakaazi walio wengi katika jimbo la Pandani, bei ya shilingi 4,000/= bado ni ghali na baada ya kuwasilisha kilio chao kwa viongozi wa Kitaifa, waliahidiwa punguzo ili iwe shilingi 2,000/= tu kwa mwezi kwa wakaazi wa vijijini. Hata hivyo, hadi sasa ahadi hii haijatekelezwa.

- (a) Je, ni kwa nini ahadi hii haijatekelezwa na lini itatekelezwa.
- (b) Je, Serikali haioni ulazima wa kupunguza bei ya maji kutoka shilingi 4,000/= hadi shilingi 2,000/= kwa wananchi wote hasa kwa vile kwa kiasi kikubwa maji yanapatikana kwa chini ya asilimia 50 ya muda.
- (c) Je, ni upi utaratibu wa kutowalipisha wananchi ambao hawapati maji kabisa katika maeneo yao.

**II. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,  
 31 Mei, 2022.



(Raya Issa Msellel)  
**KATIBU WA BARAZA**